# HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

## MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA FM – HOTEL (NJOMBE) TAREHE 11/06/2014

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma A. Kimisha | - | Diwani Kata ya Kisuke – Mwenyekiti |
| 2. | “ Tabu Katoto | - | Diwani Kata ya Igunda– Makamu M/kiti |
| 3. | “ Joseph Masaluta | - | Diwani Kata ya Bulungwa |
| 4. | “ Pili E. Sonje | - | Diwani Kata ya Ushetu |
| 5. | “ Kulwa D. Shoto | - | Diwani Kata ya Bukomela |
| 6. | “ Sospeter Bunende | - | Diwani Kata ya Idahina |
| 7. | “ Eva Pius Mkonya | - | Diwani Viti Maalum |
| 8. | “ Silyvester J. Jilala | - | Diwani Kata ya Mapamba |
| 9. | “ Sayi G. Gamaya | - | Diwani Kata ya Ukune |
| 10. | “ Esther M. Imambo | - | Viti Maalum Bulungwa |
| 11. | “ Doa M. Limbu | - | Diwani Kata ya Nyankende |
| 12. | “ Benedicto Mabuga | - | Diwani Kata ya Mpunze |
| 13. | “ Kulwa D. Nyiriga | - | Diwani Kata ya Ulewe |
| 14. | “ Damas Joseph | - | Diwani Kata ya Chambo |
| 15. | “ Emmanuel Makashi | - | Diwani Kata ya Sabasabini |
| 16. | “ Mary Lundalila | - | Viti Maalum Ushetu |
| 17. | “ Paschal Mayengo | - | Diwani Kata ya Ulowa |
| 18. | “ Emmanuel Nding’wa | - | Diwani Kata ya Kinamapula |
| 19. | “ Hamisi Majogoro | - | Diwani Kata ya Ubagwe |
| 20. | “ Mohamed Mwarabu | - | Diwani Kata ya Chona |

WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Pastory Nyororo | - | Diwani Kata ya Igwamanoni – Kwa taarifa |
| 2. | “ Paul Magazi | - | Diwani Kata ya Uyogo – Kwa taarifa |
| 3. | “ James D. Lembeli | - | Mbunge Jimbo la Kahama – Kwa taarifa |

WATAALAM

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Isabela Chilumba | - | Mkurugenzi Mtendaji (W)- Katibu |
| 2. | “ Elinight Mmari | - | Afisa Ugavi |
| 3. | “ Neuster James | - | Mwanasheria (W) |
| 4. | “ Selestine Lufundisha | - | Kaimu Afisa Biashara (W) |
| 5. | “ Egidius Kahendaguza | - | Kaimu Afisa Utumishi (W) |
| 6. | “ Deogratius Rugangila | - | Afisa Ushirika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Ndg. Kawishe Lucas | - | Kaimu Afisa Ufugaji Nyuki (W) |
| 8. | “ Jacqueline Ntulo | - | Afisa Elimu Msingi (W) |
| 9. | “ Joseph Gwassa | - | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 10. | “ Maganga C.E | - | Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 11 | Dr. Samwel Mihulu | - | Kny: Mganga Mkuu (W)) |
| 12. | Eng. Charles Pambe | - | Mhandisi wa Maji(W) |
| 13. | Ndg. Anna Ngongi | - | Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika(W) |
| 14. | “ Deus Kakulima | - | Kaimu Afisa Mifugo (W) |
| 15. | “ Philipo Karol | - | Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 16. | “ Jackson Wanyancha | - | Kaimu Afisa TEHAMA (W) |

WAGENI WAALIKWA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mwl. Shija J. Nkagi | - | Mkuu wa Shule, Kisuke Sekondari |
| 2. | “ Migebo D. Kasanda | - | Mkuu wa Shule, Kinamapula Sekondari |
| 3. | “ Cesilia Mashishanga | - | Mwalimu Mkuu S/M Italike |
| 4. | “ Juma H. Mwibombi | - | Mwalimu Mkuu S/M Iramba |
| 5. | Ndg. Greyson Kakulu | - | Mwandishi wa Habari TBC-Shinyanga |

SEKRETARIETI

Ndg. Chamo Mashauri - Mwandishi wa kikao

MUHT. NA. BM/05/2014 – KUFUNGUA KIKAO

Katibu aliwakaribisha wajumbe na wataalamu katika kikao hicho. Alieleza kuwa kikao hicho ni maalum kwa ajili ya kupitia na kujadili Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu za mwaka 2014.

Mwenyekiti alieleza kuwa kanuni hizi ziliwasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani tarehe 10-11/02/2014 ili zijadiliwe lakini hazikujadiliwa kutokana na maelezo ya waheshimiwa madiwani kuwa hawajazisoma vyema kanuni hizo. Alieleza kuwa katika kikao hicho iliazimia kuwa kanuni hizo zitajadiliwa katika kikao kingine cha kawaida au kikao maalum. Alieleza kuwa anaimani wajumbe wamesoma kanuni hizo kwa kina kwani wamekuwa na kabrasha la kanuni za kuduma tangu mwezi Februari 2014.

Aidha, mwenyekiti aliwapongeza wakuu wa shule za msingi na sekondari ambao shule zao zimefanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa taifa mwaka 2013 na kupendekezwa kushiriki katika ziara ya kujifunza ya Baraza la Madiwani mkoani Njombe hali iliyowawezesha pia kushiriki kikao hicho cha Baraza la Madiwani.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 04:27 asubuhi.

MUHT. NA. BM/06/2014 – KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU ZA MWAKA 2014

Mwanasheria (W) aliwasilisha taarifa ya kanuni hizo. Alisema kuwa Kanuni za Kudumu zinazotumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu zilitungwa na iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama mwaka 2003 . Alisema kuwa Sheria za Serikali za Mitaa zinazipa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) madaraka ya kutunga Kanuni za Kudumu za Halmashauri ambazo hutumika katika kusimamia uitishaji, usimamizi na uendeshaji wa mikutano (sura 287/2002 kifungu 70(1). Alitaja sababu za kuboresha Kanuni za Kudumu zilizopo kuwa ni:-

- Taratibu za kuzingatia wakati wa Baraza kujadili hoja ya kumwondoa Mwenyekiti wa Halmashauri kutokuwa bayana.
- Kutoeleza taratibu bora za kupiga kura katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa Halmashauri.
- Kanuni kutoeleza nini kifanyike endapo akidi ya kikao au mkutano haikutimia.
- Taratibu za kuandaa na kutoa taarifa za maendelo kutoka kwenye Kata kutokuwa bayana
- Taratibu za kuuliza na kujibu maswali ya papo kwa papo
- Muundo wa Kamati ya Fedha kwa Halmashauri zenye madiwani zaidi ya 20.
- Kanuni kuwa kimya kuhusu Kamati nyingine kutembelea miradi mbalimbali
- Kutotoa maelekezo kuhusu sala/dua kabla ya kuanza shughuli za mikutano ya Halmashauri.

Alieleza kuwa mabadiliko makubwa katika kanuni za kudumu za Halmashauri za mwaka 2014 za mfano (code/council standing orders) zilizoandaliwa na TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wengine yapo katika mambo yafuatayo:-

- Utaratibu wa kushughulikia hoja ya kumuondoa madarakani Mwenyekiti wa Halmashauri.
- Utaratibu mpya wa akidi
- Utaratibu mpya wa kupiga kura za kumchagua mwenyekiti
- Utaratibu wa kutoa taarifa kutoka kwenye Kata
- Utaratibu wa maswali ya papo kwa papo
- Muundo wa Kamati za Fedha za Halmashauri.

Maamuzi yote ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanywa kupitia vikao na mikutano ya Halmashauri na kwamba kuwepo kwa kanuni za kudumu za mwaka 2014 kutabadilisha na kuboresha mfumo wa uitishaji na uendeshaji wa vikao na mikutano ya Halmashauri.

Baada ya kuwasilisha, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Doa Limbu alieleza kuwa katika kanuni ya 40 (2) kinaeleza kuwa “wajumbe wengine wasiozidi wawili watapendekezwa na mwenyekiti na kupigiwa kura na Baraza la Halmashauri, mmoja kati yao awe mwanamke” alieleza kuwa kitendo cha kupiga kura kitasababisha wajumbe waliopendekezwa kutoa rushwa ili wapigiwe kura. Alishauri kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ateue wajumbe hao wa Kamati lakini wasipigiwe kura na Baraza la Halmashauri.

Mhe. Emmanuel Makashi aliunga mkono kanuni ya 40 kama ilivyowasilishwa. Alieleza kuwa iwapo majina ya wajumbe wa Kamati walioteuliwa na Mwenyekiti hayataridhiwa na Baraza la Halmashauri kwa kupigiwa kura, basi Mwenyekiti wa Halmashauri atateua jina au majina mengine hadi pale Baraza la Halmashauri litakaporidhia majina yaliyopendekezwa kwa njia ya kupiga kura. Alisema kuwa demokrasia ya kweli ni ile inayomshirikisha mhusika moja kwa moja.

Mhe. Paschal Mayengo alisema kuwa ni haki ya msingi Mwenyekiti wa Halmashauri kupewa mamlaka ya kuteua wajumbe wawili wa kamati ya Fedha, Utawala na Mipango na wajumbe hao wasipigiwe kura. Alieleza kuwa Mwenyekiti huchaguliwa na wajumbe wa Baraza la Madiwani hivyo wanamwamini.

Mhe. Esther Imambo aliunga mkono maoni yaliyotolewa na Mhe. Doa Limbu na Mhe. Paschal Mayengo na kusema kuwa Mwenyekiti apewe uhuru wa kuteua wajumbe hao na siyo kupendekeza kisha Baraza la Madiwani lithibitishe kwa kupiga kura .

Mhe. Sospeter Bunende alieleza kuwa baada ya Mwenyekiti kuteua wajumbe wa Kamati kusiwe na upigaji kura kuthibitisha wajumbe hao. Aidha alieleza kuwa suala la upigaji kura likifanyika litasababisha kuvinyima fursa vyama ambavyo havina wajumbe wengi wa Baraza la Halmashauri kwani hata wakipendekezwa na Mwenyekiti hawatapata kura za kutosha kuteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati.

Mhe. Pili Sonje aliunga mkono wazo la Mhe. Sospeter Bunende ili kuondoa mivutano isiyo na tija wakati wa vikao vya Baraza la Madiwani. Alieleza kuwa kanuni hizi za Halmashauri za mwaka 2014 zinalenga kutumika kwa miaka mingi na siyo mwaka mmoja. Pia aliunga mkono mawazo ya Mhe. Doa Limbu.

Mhe. Kulwa Shoto alieleza kuwa ili kuepusha wajumbe wa kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kujirudia kila mwaka, alishauri kuwa mwenyekiti ateue majina ya wajumbe kisha yathibitishwe na Baraza la Madiwnai kwa njia ya kupiga kura.

Mhe. Emmanuel Nding’wa aliunga mkono maoni ya Mhe. Kulwa Shoto kuwa baada ya Mwenyekiti kuteua wajumbe wa kamati, wathibitishwe na Baraza la Madiwani kwa njia ya kura.

Mhe. Mohamed Mwarabu alieleza kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri huwa ni diwani aliyechaguliwa na wananchi na hupewa madaraka ya uenyekiti kupitia kura zinazopigwa na wajumbe wa Baraza la Madiwani, kwa mantiki hiyo Mwenyekiti huwa na hekima na busara na ni mtu anayeaminika. Alishauri kuwa wajumbe wa kamati watakaoteuliwa na mwenyekiti wasipigiwe kura.

Mhe. Joseph Masaluta alieleza kuwa ili taarifa mbalimbali za Kamati ya Maadili ziweze kujadiliwa au kufafanuliwa kwa kina, Mwenyekiti wa Kamati hiyo anatakiwa kuwa mjumbe wa kamati ya Fedha, Utawala na Mipango. Aidha alisema kuwa ajenda za mkutano wa Baraza la Madiwani hupangwa na kamati ya Fedha, Utawala na Mipango hivyo kama kutakuwa na ajenda inayotoka Kamati ya Maadili, atakosekana mjumbe wa kuifafanua.

Mhe. Benedicto Mabuga alisema kuwa kanuni ya 40 (1) inataja Kamati tano za Kudumu za Halmashauri ikiwa ni pamoja na Kamati ya Maadili na kwamba kifungu cha (2) kinaeleza kuwa wajumbe wa Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango. Alitaka kujua kwanini kwa sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili siyo mjumbe wa kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Halmashauri za mwaka 2014 ambazo zinajadiliwa katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili  atakuwa wajumbe wa Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.

Mhe. Sayi Gamaya alisema kuwa kanuni zinaelekeza kuwa iwapo mjumbe hatahudhuria vikao vitatu mfululizo atakuwa amejifuta kwenye madaraka yake ya udiwani, lakini kanuni ya 17 (2) inampa Mwenyekiti wa Baraza mamlaka ya kumwondoa au kumzuia kuhudhuria vikao vitatu mfululuzo mjumbe atakayesababisha fujo hata baada ya kukanywa akaendelea kukaidi. Alisema maelezo ya kanuni hizo yanakinzana hivyo alitaka ufafanuzi.

Aidha kanuni ya 25 inaeleza kuhusu taarifa za kutoka kwenye Kata. Alisema kuwa kanuni ya 25 (2) inaeleza kuwa taarifa hizo zitawasilishwa na Diwani wa Kata husika. Alitaka kujua kwa nini taarifa za kutoka kwenye Kata ziandaliwe na Afisa Mtendaji wa Kata halafu ziwasilishwe na Diwani wa Kata.

Mwanasheria (W) alifafanua kuwa Diwani akiacha kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila taarifa ndiyo atakuwa amejifuta kwenye madaraka yake ya udiwani. Kwa kuwa kutokuwepo kwa diwani katika vikao vitatu mfululizo kama adhabu ni suala linalotambukilika na lililoamuliwa kikaoni, Diwani huyo atahesabika kutokuwepo kikao ni kwa taarifa.

Kuhusu kuandaa na kuwasilisha taarifa kutoka katani alieleza kuwa Mwenyekiti (Diwani) na Katibu (Afisa Mtendaji wa Kata) wa WDC kwa pamoja wataandaa

taarifa waliyotekeleza ndani ya Kata yao ambayo itawasilishwa na Mheshimiwa Diwani katika vikao vya Baraza la Halmashauri.

Baada ya mjadala huo, Mwenyekiti alieleza kuwa wajumbe wengi waliochangia maoni yao kuhusu Kamati za Kudumu na wajumbe wawili wa Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango waliotajwa kwenye kanuni ya 40 (2) wametoa maoni yao kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri akishateua wajumbe hao, atawasilisha majina kwenye kikao cha Baraza la Halmashauri na hawatapigiwa kura kuthibitishwa kutokana na sababu zifuatazo:-

- Kitendo cha kupiga kura kitasababisha wajumbe waliopendekezwa kutoa rushwa ili wapigiwe kura.
- Suala la upigaji kura likifanyika litasababisha kuvinyima fursa vyama ambavyo havina wajumbe wengi wa Baraza la Halmashauri.
- Mwenyekiti huwa na hekima na busara, anaaminika na amepewa madaraka ya uenyekiti na wajumbe wa Baraza la Halmashauri kwa njia ya kura hivyo uteuzi wake uthaminiwe na kuaminiwa.

MUHT. NA. BM/07/2014 – KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao ya mawazo na kuwapongeza kwa ushirikiano wanaouonesha tangu kuanzishwa kwa Halmashauri mpya ya Wilaya ya Ushetu Juni 2013. Alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji (W) na wataalam kwa utekelezaji mzuri wa majukumu ya Halmashauri huku wakishirikiana bega kwa bega na waheshimiwa Madiwani. Alimpongeza Kaimu Afisa Ugavi (W) kwa kuandaa semina fupi kuhusu Matumizi ya Sheria mpya ya Manunuzi Na.7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake GN 446 za mwaka 2013 iliyofanyika asubuhi kabla ya kuanza kwa kikao Maalum cha Baraza la Madiwani. Alifunga kikao saa 09:49 alasiri.

MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA

NA

| | | |
|---|---|---|
| ..... | ..... | ..... |
| Isabela O. Chilumba | | Juma A. Kimisha |
| KATIBU | TAREHE | MWENYEKITI |